**Learning by Ear**

**People Who Make a Difference**

**Long Run For Life (Ethiopia)**

Author: Alexander Göbel

Editor: Stefanie Duckstein, Jan-Philipp Scholz

Proof Reader: Anthony Dunham

Sound clips in DALET: Learning by Ear-Folder – “LBE_PEO_etc.”

CHARACTERS:

Announcer: Male/Female

Sound clips: Toshome Shumi (male, 16)
Merert (female, 16)

**INTRO (Announcer):**

Hujambo msikilizaji na karibu kwenye Noa Bongo Jenga Maisha Yako kwa jina” Watu Wanaoleta Mabadiliko katika Jamii“, makala haya yanakuwezesha kukutana na mashujaa wa kawaida katika maisha barani Afrika. Watu hao ni jasiri, wakweli na pia ni watu wenye msimamo. Watu hao wana muongozo wa maisha ya baadae na pia wana imani kubwa na ndoto walizonazo maishani. Leo utakutana na Toshome, kijana wa Kiethiopia anayejitahidi kuwa mkimbiaji maarufu.

**TEXT:**

*1. SFX: Village, Horse*

Ni saa kumi na mbili asubuhi. Ni alfajiri iliyo kimya na ukungu umetanda kila mahala. Nje kuna wakulima wachache wanaoelekea kwenye mashamba yao, wakiwa na punda wao wadogo tena waliokonda wakivuta makwama kwenye barabara iliyojaa tope.

*2. SFX: Running*

Na hapo hapo kuna mvulana mmoja mdogo ameyevaa gwanda lililoraruka na viatu vibovu, anashindana na punda wengine huku yeye akiwa juu ya gari linalovutwa na punda wawili , halafu kwa urahisi anawapita wale punda wengine mmoja baada ya mwingine. Uso wake umejawa na tabasamu huku anawapungia mkono wakulima kila anapowapita. Kijana huyu ni mtu mwenye aibu sana kwani hajawahi kuzungumza na watu asiowajua – lakini ifikiapo kwenye mchezo anaoupenda basi kijana huyu alikuwa tayari kabisa kuvunja kimya chake:

*3. Sound Bite Toshome:*

*"Jina langu ni Toshome Shumi. Nina miaka 16 na ninataka kuwa mwanariadha. Wazazi wangu wameshafariki dunia, hiyo ni habari ya kusikitisha. Lakini kila ninapokimbia mimi husahau shida zangu zote.*

*Napenda sana kukimbia."*

Tuko katika kijiji kidogo cha Saguree, kilicho katika nyanda za juu za Ethiopia, sehemu yenyewe iko kati ya Asela na Bokoji. Inachukua zaidi ya siku moja kusafiri hadi mji mkuu wa Addis. Kwa watu wanaoishi katika vilima vya Arsi, itabaki kuwa ndoto na wala haitowezekana, kwamba siku moja wataweza kuukanyaga mji mkuu wa Addis na ahadi zake za maisha bora ya siku za usoni.

*4. SFX: Running (use where find appropriate)*

Nyanda za juu zinasifika kwa kutoa wanariadha maarufu. Pia utafiti wa kibiolojia unaonyesha kuwa, sehemu za juu zenye urefu wa mita 2500, zinachangia katika kujengeka chembe nyekundu za damu. – kwa kadri mtu anavyokuwa na chembe nyekundu nyingi ndivyo mwili wake unavyokuwa na hewa safi ya oksijeni. Inakuwa kama njia asilia ya kuongeza nguvu mwilini. Kwa mujibu wa wataalamu wa tiba, mwili wa mwanadamu unanufaika kwa njia nyingi kutokana na kukimbia lakini sio kwa kupita kiasi. Faida zenyewe ni pamoja na kupunguza uzito mwilini kwa kiasi kikubwa, kupunguza hatari ya magonjwa ya moyo, kupunguza mlimbikizo wa misuli na matatizo ya mifupa. Kukimbia kunaleta furaha moyoni.

Kwa mkimbiaji wa kulipwa mazingira yasingeweza kuwa mabaya kuliko katika maeneo ya Saguree. Kijiji hicho ni kati ya vijiji masikini katika jimbo hilo, eneo hilo halina umeme wala maji ya bomba,

usambe barabara. Hata magari yenye nguvu yanakwama kila siku. Saguree haina klabu ya michezo, haina vifaa vya michezo na wala hakuna makocha pia. Kwa sababu zote hizo Toshome havunjiki moyo. Kijana huyo amejitolea kupambana kwa kile anachokiamini – kwa hali yoyote ile.

*5. Sound Bite Toshome:*

*Wakati mwingine rafiki zangu wanajiunga nami. Lakini mara nyingi ninafanya mazoezi peke yangu. Mimi sijali, wajua! Mimi napenda kuwa peke yangu. Ninaamini nitafaulu, kutakuwa na mashindano ya mkoa wakati wa kiangazi.*

Leo rafiki yake anaeitwa Merert amejiunga nae – yeye ana miaka 16 na ndoto yake ni kama ya Toshome, wote wana kiu cha kuwa wakimbiaji.

6. *Sound Bite Merert*

*Nikikimbia huwa nawafikiria wale wanariadha maarufu wanaonivutia kutoka nyanda za juu. halafu, mimi husahau kila kitu, husahau tabu zangu zote na hapo hujisikia mwepesi sana. Nafurahia sana kukimbia hata nikiwa sijakula kitu.*

Katika wiki chache zijazo mashindano ya kusaka vipaji ya Addis yatafanyika tena katika maeneo ya nyanda za juu na mara hii kijana Toshome anatarajia kuwa kipaji chake kitaonekana na kwamba yeye ni mkimbiaji wa kutegemewa katika mbio za mita 5000 na mita 10.000.

Yeye ni kati ya maelfu ya vijana wa Kiethiopia wanaotafuta nafasi katika Klabu za michezo. Vijana hao wote wanatamani angalau wapate malipo japo kidogo pindi watakapochukuliwa na Klabu yoyote. Vijana hao pia wanatarajia kuwa na maisha mazuri pindi watakapochaguliwa. Toshome ana ndoto kama vijana hao wenzake ila yeye ni tafauti. Yeye ni mmoja tu kati ya mamilioni kwa sababu yuko peke yake. Yeye hana njia nyingine yoyote isipokuwa kukimbia tu.

*7. Sound Bite Toshome:*
*Mimi huamka saa kumi na moja na nusu alfajiri, nikisha usafisha mwili wangu mara moja naanza mazoezi mpaka saa mbili asubuhi na hapo ninakwenda zangu shule.*

Shule anayosoma iko umbali wa kilomita 10 – na bila shaka kijana Toshome anahitajika kukimbia kuelekea huko shule. Japo ana miaka 16, bado yuko darasa la tano. Wazazi wake walifariki dunia akiwa bado mdogo – anasema wazazi wake walipewa sumu. Toshome hapendi sana kuzungumzia swala hilo na anainamisha kichwa chake chini. Machozi yanamtoka, lakini kwa haraka anayapangusa.

*8. Sound Bite Toshome*
*Mara nyingine nawafikiria sana wazazi wangu ...bila shaka wangejivunia sana. Kusema kweli ndugu zangu wako na wanafanya kila jitihada kunisaidia. Lakini msaada wa wazazi wangu ungefanya nipate mafanikio kwa urahisi.*

*9. Music Interlude (1:00 min - 1:30 min); suggestion: Astatke, Mulatu*

Toshome anaishi na kaka yake mkubwa katika shamba lake huko magharibi mwa Saguree. Anaishi pamoja na familia ya kaka yake kwenye kijumba kidogo cha matope; mke wa kakake na watoto wao watatu. Hakika hapo sio kabisa mahala ambapo mwanariadha mashuhuri mtarajiwa anapostahili kuishi maisha yake yote.

*10. Sound Bite Toshome*
*Nikipata fedha nitazihifadhi kwa ajili ya kununua viatu vizuri vya kukimbilia.*

Viatu anavyovaa Toshome kwa sasa havistahili kabisa kuitwa viatu. Vimepasuka na vina matundu kwenye nyayo wakati akitembea vinaachana. Toshome amevibandika kwa gundi viatu vyake mara nyingi. Alivinunua vikiwa tayari vimeshatumiwa na vilimgharimu kiasi cha Euro 8. Hizo ni pesa nyingi ambazo zilimlazimu kufanya kazi ngumu kwa miezi miwili. Alifanya kazi ya kibarua katika shughuli za ujenzi, alichunga ng'ombe, alisafisha na kupiga rangi viatu na hata alifanya kazi katika mkahawa wa chai kijijini hapo. Yeye angependa sana kuwa tarishi wa meya wa jiji. Ni mtu wa kutegemewa, mwaminifu na anafanya kila kitu kwa bidii kubwa zaidi. Kila kazi inamuongezea mazoezi ya kukimbia kilomita kadhaa za ziada na wala hajali barabara mbaya za kijiji cha Saguree.

*11. Sound Bite Toshome*

*Viatu hivi vitanisaidia kwa miezi mingine miwili au mitatu. Lazima iwe hivyo kwa sababu sina vingine. Na hii suruali yangu nyekundu ndio nguo peke yake niliyonayo – sina nyingine.*

Toshome anafanya mazoezi ya mbio za mita 10.000 na pia mbio za nusu marathon ambazo ni kilomita 21, lakini mbio anazopendelea sana ni mbio za urefu wa mita 5000, yeye humaliza mbio hizo kwa dakika 15, tena kwenye barabara za matope za kijijini. Rekodi ya dunia ambayo kwa kawaida hufanyika kwenye mahala tambarare ilichukua muda wa chini ya dakika 13 – Mkimbiaji maarufu anaependwa sana na kijana Toshome Muethiopia Kenenisa Bekele ndie aliyevunja rekodi hiyo. Bekele alichukua nafasi ya mwanariadha maarufu bingwa wa dunia wa zamani, Haile Gebreselassie. Yeye anatoka katika jimbo la Arsi.

*12. Sound Bite Toshome*
*Amini, usiamini – siku moja nitakuwa kama Kenenisa. Nitavaa sare ya taifa na nitajiunga na kikosi cha taifa. Nitafaulu.*

*13. SFX: Stadium, Cheering Crowds, Running*

Na kweli alifaulu. Baada ya wiki chache tumepokea barua kutoka kwa Toshome. Kijana huyo ameeleza kuwa alishinda katika mashindano ya mkoa mwezi mmoja baada ya sisi kumtembelea huko maeneo ya nyanda za juu. Mvulana huyo mwenye aibu ameshaondoka kutoka kijiji cha Saguree akiwa tayari kabisa kuwa mwanariadha mashuhuri.

Sasa anaishi na mlezi wake ambae ni rafiki ya baba yake katika jiji la Addis na pia ameshajiunga na klabu ya wanariadha inayojulikana. Toshome ametutumia picha inayoonyesha amevaa jezi ya taifa. Ama kweli ndoto ya Toshome imeanza kuwa kweli. Bila shaka tutamuona kijana huyu kwenye mashindano ya olimpiki hivi karibuni hata yeye mwenyewe anatarajia hivyo hivyo.

*14. Sound Bite Toshome*

*Mimi hujawa na furaha nikikimbia. Hujihisi kama ninaruka. Siku moja ikipita bila ya kukimbia, hiyo huwa ni siku mbaya. Unajua?*

*14. SFX: Crowds cheering, Ethiopian National Anthem*

**OUTRO (Announcer):**

Hiyo ilikuwa ni hadithi ya Toshome, kijana mwanariadha mwenye umri wa miaka 16 – ambaye pamoja na hali ngumu aliyokuwa nayo – alitambua wazi kitu alichokitaka maishani mwake na hakusita kukipigania tena kwa bidii zote. Ana dhamira ya kuiga mifano ya mashujaa wa taifa la Ethiopian kama Haile Gebreselassie, Kenenisa Bekele au Tirunesh Dibaba. Je wewe unamfikiriaje kijana huyu? Iwapo ungependa kutupa maoni yako basi jielimishe zaidi juu ya swala hili au sikiliza tena kipindi hiki. Anwani yetu ya mtandao ni www.dw-world.de/lbe. Asante kwa kusikiliza na ni matumaini yangu kuwa tutaungana tena wakati mwingine katika hadithi zingine za Noa Bongo Jenga Maisha Yako kwenye mfululizo wa hadithi kuhusu watu wanaoleta Mabadiliko. Hadi hapo, Kwaheri.